JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA MAJI

MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI (EWURA)

***KUMB: PPR/2021 - 03/1***

**TAARIFA KWA UMMA KUHUSU BEI KIKOMO ZA BIDHAA ZA MAFUTA YA PETROLI KUANZIA JUMATANO, TAREHE 3 MACHI 2021**

Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), inatangaza bei kikomo za bidhaa za mafuta ya petroli hapa nchini. Bei hizi zitaanza kutumika kuanzia **Jumatano, Tarehe 3 Machi 2021.** Pamoja na kutambua bei hizo, ni muhimu kuzingatia yafuatayo:-

(a) Bei za rejareja na jumla za mafuta ya Petroli, Dizeli na Mafuta ya Taa yaliyopokelewa kupitia **Bandari ya Dar es Salaam** zimeongezeka ikilinganishwa na toleo lililopita la tarehe 3 Februari 2021. Kwa Machi 2021, bei za rejareja za Petroli, Dizeli na Mafuta ya Taa zimeongezeka kwa shilingi 94/Lita (sawa na asilimia 4.99), shilingi 82/Lita (sawa na asilimia 4.47) na shilingi 94/Lita(sawa na asilimia 5.34), mtawalia. Vilevile, ikilinganishwa na toleo la mwezi uliopita, bei za jumla za Petroli, Dizeli na Mafuta ya Taa zimeongezeka kwa shilingi 93.77/Lita (sawa na asilimia 5.33), shilingi 81.38/Lita (sawa na asilimia 4.78) na Shilingi 94.16/lita (sawa na asilimia 5.74), mtawalia.

(b) Kwa Machi 2021, bei za jumla na rejareja kwa mafuta ya Petroli na Dizeli **kwa Mikoa ya Kaskazini** (Tanga, Kilimanjaro, Arusha na Manyara) zimeongezeka ikilinganishwa na bei zilizotolewa tarehe 3 Februari 2021. Kwa mwezi Machi 2021, bei za rejareja za Petroli na Dizeli zimeongezeka kwa shilingi 163/lita (sawa na asilimia 8.47) na shilingi 85/lita (sawa na asilimia 4.64), mtawalia. Vilevile, ikilinganishwa na toleo la mwezi uliopita, bei za jumla za Petroli na Dizeli zimeongezeka kwa shilingi 162.12/Lita (sawa na asilimia 9.05) na shilingi 84.80/lita (sawa na asilimia 4.97) mtawalia. Hata hivyo, bei za Mafuta ya Taa hazina mabadiliko na zitaendelea kuwa zile zilizotangazwa katika toleo la tarehe 3 Februari 2021. Hii ni kwa sababu, kwa Februari 2021 hakuna shehena ya Mafuta ya Taa iliyopokelewa kupitia bandari ya Tanga.

(c) Kwa Machi 2021, bei za rejareja na jumla kwa bidhaa za mafuta ya Petroli na Dizeli **kwa Mikoa ya Kusini** (**Mtwara, Lindi, and Ruvuma**) zitaendelea

kuwa zile zilizotangazwa katika toleo la tarehe 3 Februari 2021. Hii ni kwa sababu, kwa mwezi Februari 2021 hakuna shehena ya Mafuta iliyopokelewa kupitia bandari ya Mtwara.

(d) Mabadiliko haya ya bei yanachangiwa na kubadilika kwa bei za mafuta katika soko la dunia na gharama za usafirishaji (*BPS Premium*).

(e) EWURA inapenda kuukumbusha umma kwamba bei kikomo za bidhaa za mafuta ya petroli kwa eneo husika zinapatikana pia kupitia simu za mkononi kwa kupiga namba ***152*00#** na kisha kufuata maelekezo. Huduma hii ni bure na inapatikana kupitia mitandao yote ya simu za mkononi hapa nchini.

(f) Kwa mujibu wa **Sheria ya Mafuta ya mwaka 2015, kifungu namba 166**, bei za bidhaa za mafuta ya petroli zitaendelea kupangwa na soko. EWURA itaendelea kuhamasisha ushindani kwa kutoa taarifa za bei kikomo za bidhaa za mafuta. Taarifa hizi zina lengo la kuwasaidia wadau kufanya maamuzi stahiki kuhusu manunuzi ya bidhaa za mafuta.

(g) Kampuni za mafuta ziko huru kuuza bidhaa za mafuta ya petroli kwa bei ya ushindani mradi tu **bei hizo zisivuke bei kikomo (*price cap*) kama ilivyokokotolewa na kanuni (*formula)* iliyopitishwa na EWURA na ambayo ilichapishwa katika Gazeti la Serikali Na. 656 la tarehe 21 Agosti 2020**.

(h) Vituo vyote vya mafuta vinatakiwa kuchapisha bei za bidhaa za mafuta katika mabango yanayoonekana bayana na yakionesha bei ya mafuta, punguzo, vivutio vya biashara au promosheni zinazotolewa na kituo husika. Pale ambapo inawezekana kuchagua, wateja wanashauriwa kununua bidhaa za mafuta katika vituo vinavyouza mafuta kwa bei nafuu zaidi ili kushamirisha ushindani. **Ni kosa kuuza mafuta bila kuweka mabango ya bei inayoonekana vizuri kwa wateja. Adhabu kali itatolewa kwa kituo husika kwa kutotekeleza matakwa ya kisheria kwa mujibu wa kanuni husika.**

(i) Wauzaji wa mafuta ya petroli wanatakiwa kutoa risiti za mauzo kutoka kwenye mashine za EFPP (*Electronic Fiscal Pump Printers*) na Wanunuzi wahakikishe wanapata stakabadhi hizo za malipo zinazoonyesha jina la kituo, tarehe, aina ya mafuta yaliyonunuliwa na bei kwa lita. Stakabadhi hizo za malipo zitatumika kama kidhibiti kwa wanunuzi wa mafuta endapo kutajitokeza malalamiko ya aidha kuuziwa mafuta kwa bei ya juu kuliko bei kikomo au kuuziwa mafuta yasiyo na kiwango cha ubora kinachofaa, na pia, risiti hizo zitasaidia kurahisisha ukusanyaji wa kodi za Serikali zitokanazo na mauzo ya mafuta ya petroli.

## JEDWALI A: BEI ZA REJAREJA

| **Mji** | **Bei Kikomo** | | |
|---|---|---|---|
| | **Petroli (Shs/Lita)** | **Dizeli (Shs/Lita)** | **Mafuta Ya Taa (Shs/Lita)** |
| **Dar es Salaam** | **1,981** | **1,911** | **1,863** |
| **Arusha** | **2,139** | **1,975** | **2,051** |
| Arumeru (Usa River) | 2,139 | 1,975 | 2,051 |
| Karatu | 2,157 | 1,994 | 2,069 |
| Longido | 2,150 | 1,986 | 2,062 |
| Monduli | 2,144 | 1,981 | 2,056 |
| Monduli-Makuyuni | 2,149 | 1,985 | 2,061 |
| Ngorongoro (Loliondo) | 2,223 | 2,060 | 2,136 |
| **Pwani (Kibaha)** | **1,985** | **1,915** | **1,868** |
| Bagamoyo | 1,992 | 1,922 | 1,874 |
| Bagamoyo (Miono) | 2,023 | 1,953 | 1,905 |
| Chalinze Junction | 1,995 | 1,925 | 1,878 |
| Chalinze Township (Msata) | 1,999 | 1,929 | 1,882 |
| Kibiti | 2,001 | 1,931 | 1,884 |
| Kisarawe | 1,988 | 1,918 | 1,871 |
| Mkuranga | 1,991 | 1,921 | 1,873 |
| Rufiji | 2,008 | 1,938 | 1,891 |
| **Dodoma** | **2,040** | **1,970** | **1,922** |
| Bahi | 2,047 | 1,977 | 1,929 |
| Chamwino | 2,035 | 1,965 | 1,917 |
| Chemba | 2,066 | 1,996 | 1,949 |
| Kondoa | 2,072 | 2,002 | 1,955 |
| Kongwa | 2,037 | 1,967 | 1,919 |
| Mpwapwa | 2,041 | 1,971 | 1,923 |
| Mtera (Makatopora) | 2,058 | 1,989 | 1,941 |
| Mvumi | 2,046 | 1,976 | 1,929 |
| **Geita** | **2,146** | **2,076** | **2,029** |
| Bukombe | 2,135 | 2,065 | 2,018 |
| Chato | 2,167 | 2,097 | 2,050 |
| Mbogwe | 2,184 | 2,114 | 2,067 |
| Nyang'hwale | 2,161 | 2,091 | 2,044 |
| **Iringa** | **2,045** | **1,975** | **1,928** |
| Ismani | 2,050 | 1,980 | 1,933 |

| Mji | Bei Kikomo | | |
|---|---|---|---|
| | **Petroli (Shs/Lita)** | **Dizeli (Shs/Lita)** | **Mafuta Ya Taa (Shs/Lita)** |
| Kilolo | 2,049 | 1,979 | 1,932 |
| Mufindi (Mafinga) | 2,055 | 1,985 | 1,938 |
| Mufindi (Igowole) | 2,064 | 1,994 | 1,946 |
| **Kagera (Bukoba)** | **2,196** | **2,126** | **2,079** |
| Biharamulo | 2,171 | 2,101 | 2,053 |
| Karagwe (Kayanga) | 2,213 | 2,143 | 2,095 |
| Kyerwa (Ruberwa) | 2,218 | 2,149 | 2,101 |
| Muleba | 2,196 | 2,126 | 2,079 |
| Ngara | 2,184 | 2,114 | 2,067 |
| Misenyi | 2,205 | 2,135 | 2,087 |
| **Katavi (Mpanda)** | **2,189** | **2,119** | **2,071** |
| Mlele (Inyonga) | 2,208 | 2,138 | 2,091 |
| Mpimbwe (Majimoto) | 2,182 | 2,112 | 2,064 |
| Tanganyika (Ikola) | 2,207 | 2,137 | 2,089 |
| **Kigoma** | **2,212** | **2,142** | **2,095** |
| Uvinza (Lugufu) | 2,224 | 2,155 | 2,107 |
| Buhigwe | 2,201 | 2,131 | 2,084 |
| Kakonko | 2,169 | 2,099 | 2,052 |
| Kasulu | 2,198 | 2,128 | 2,081 |
| Kibondo | 2,176 | 2,107 | 2,059 |
| **Kilimanjaro (Moshi)** | **2,128** | **1,965** | **2,041** |
| Hai (Bomang'ombe) | 2,132 | 1,968 | 2,044 |
| Mwanga | 2,121 | 1,958 | 2,034 |
| Rombo (Mkuu) | 2,145 | 1,982 | 2,057 |
| Same | 2,115 | 1,951 | 2,027 |
| Siha (Sanya Juu) | 2,135 | 1,972 | 2,047 |
| **Lindi** | **1,917** | **1,842** | **1,922** |
| Lindi-Mtama | 1,922 | 1,847 | 1,940 |
| Kilwa Masoko | 1,941 | 1,866 | 1,897 |
| Liwale | 1,953 | 1,878 | 1,943 |
| Nachingwea | 1,937 | 1,862 | 1,952 |
| Ruangwa | 1,943 | 1,869 | 1,953 |
| **Manyara (Babati)** | **2,173** | **2,009** | **2,085** |
| Hanang (Katesh) | 2,183 | 2,020 | 2,095 |
| Kiteto (Kibaya) | 2,188 | 2,025 | 2,100 |

| Mji | Bei Kikomo | | |
|---|---|---|---|
| | **Petroli (Shs/Lita)** | **Dizeli (Shs/Lita)** | **Mafuta Ya Taa (Shs/Lita)** |
| Mbulu | 2,185 | 2,022 | 2,098 |
| Simanjiro (Orkasumet) | 2,205 | 2,042 | 2,117 |
| **Mara (Musoma)** | **2,159** | **2,089** | **2,042** |
| Musoma Vijijini (Busekela) | 2,200 | 2,130 | 2,083 |
| Rorya (Ingirijuu) | 2,168 | 2,098 | 2,051 |
| Rorya (Shirati) | 2,203 | 2,133 | 2,086 |
| Bunda | 2,151 | 2,081 | 2,033 |
| Bunda (Kisorya) | 2,160 | 2,090 | 2,043 |
| Butiama | 2,156 | 2,086 | 2,039 |
| Serengeti (Mugumu) | 2,205 | 2,135 | 2,088 |
| Tarime | 2,170 | 2,101 | 2,053 |
| Tarime (Kewanja/Nyamongo) | 2,175 | 2,105 | 2,058 |
| **Mbeya** | **2,088** | **2,018** | **1,971** |
| Chunya | 2,097 | 2,028 | 1,980 |
| Chunya (Makongolosi) | 2,103 | 2,033 | 1,985 |
| Chunya (Lupa Tingatinga) | 2,105 | 2,035 | 1,987 |
| Kyela | 2,104 | 2,034 | 1,986 |
| Mbarali (Rujewa) | 2,072 | 2,002 | 1,955 |
| Rujewa (Madibira) | 2,085 | 2,015 | 1,968 |
| Rujewa (Kapunga) | 2,082 | 2,012 | 1,964 |
| Rungwe (Tukuyu) | 2,097 | 2,027 | 1,980 |
| **Morogoro** | **2,006** | **1,936** | **1,888** |
| Mikumi | 2,021 | 1,951 | 1,904 |
| Kilombero (Ifakara) | 2,044 | 1,974 | 1,926 |
| Kilombero (Mlimba) | 2,066 | 1,996 | 1,949 |
| Kilombero (Mngeta) | 2,055 | 1,985 | 1,938 |
| Ulanga (Mahenge) | 2,054 | 1,984 | 1,937 |
| Malinyi | 2,065 | 1,995 | 1,947 |
| Kilosa | 2,024 | 1,954 | 1,907 |
| Gairo | 2,024 | 1,954 | 1,907 |
| Mvomero (Wami Sokoine) | 2,016 | 1,946 | 1,899 |
| Mvomero (Sanga Sanga) | 2,006 | 1,936 | 1,888 |
| Turian | 2,031 | 1,961 | 1,914 |
| **Mtwara** | **1,903** | **1,829** | **1,936** |
| Nanyumbu (Mangaka) | 1,940 | 1,865 | 1,985 |

| Mji | Bei Kikomo | | |
|---|---|---|---|
| | Petroli (Shs/Lita) | Dizeli (Shs/Lita) | Mafuta Ya Taa (Shs/Lita) |
| Masasi | 1,920 | 1,845 | 1,962 |
| Newala | 1,924 | 1,850 | 1,968 |
| Tandahimba | 1,917 | 1,843 | 1,961 |
| Nanyamba | 1,917 | 1,843 | 1,961 |
| **Mwanza** | **2,131** | **2,061** | **2,014** |
| Kwimba | 2,149 | 2,079 | 2,031 |
| Magu | 2,139 | 2,069 | 2,022 |
| Misungwi | 2,125 | 2,055 | 2,008 |
| Sengerema | 2,163 | 2,093 | 2,046 |
| Ukerewe | 2,190 | 2,121 | 2,073 |
| **Njombe** | **2,073** | **2,003** | **1,956** |
| Njombe (Kidegembye) | 2,094 | 2,024 | 1,977 |
| Ludewa | 2,111 | 2,041 | 1,994 |
| Makambako | 2,066 | 1,996 | 1,948 |
| Makete | 2,104 | 2,034 | 1,987 |
| Wanging'ombe (Igwachanya) | 2,071 | 2,001 | 1,954 |
| **Rukwa (Sumbawanga)** | **2,154** | **2,084** | **2,036** |
| Sumbawanga Rural (Mtowisa) | 2,154 | 2,084 | 2,036 |
| Kalambo (Matai) | 2,161 | 2,091 | 2,044 |
| Nkasi (Namanyele) | 2,167 | 2,097 | 2,050 |
| **Ruvuma (Songea)** | **1,989** | **1,914** | **1,987** |
| Mbinga | 2,002 | 1,927 | 2,020 |
| Namtumbo | 1,980 | 1,905 | 2,016 |
| Nyasa (Mbamba Bay) | 2,027 | 1,952 | 2,031 |
| Tunduru | 1,954 | 1,880 | 2,046 |
| **Shinyanga** | **2,110** | **2,040** | **1,993** |
| Kahama | 2,123 | 2,053 | 2,006 |
| Kishapu | 2,138 | 2,068 | 2,021 |
| Ushetu (Nyamilangano) | 2,141 | 2,071 | 2,024 |
| Salawe | 2,124 | 2,054 | 2,007 |
| **Simiyu (Bariadi)** | **2,151** | **2,081** | **2,034** |
| Busega (Nyashimo) | 2,144 | 2,074 | 2,027 |
| Itilima (Lagangabilili) | 2,154 | 2,084 | 2,037 |
| Maswa | 2,143 | 2,073 | 2,025 |
| Meatu (Mwanhuzi) | 2,150 | 2,080 | 2,032 |

| Mji | Bei Kikomo | | |
|---|---|---|---|
| | Petroli (Shs/Lita) | Dizeli (Shs/Lita) | Mafuta Ya Taa (Shs/Lita) |
| **Singida** | **2,072** | **2,002** | **1,954** |
| Iramba | 2,084 | 2,014 | 1,966 |
| Manyoni | 2,056 | 1,986 | 1,939 |
| Itigi (Mitundu) | 2,072 | 2,002 | 1,954 |
| Ikungi | 2,067 | 1,997 | 1,950 |
| Mkalama (Nduguti) | 2,096 | 2,026 | 1,979 |
| **Songwe (Vwawa)** | **2,097** | **2,027** | **1,980** |
| Songwe (Mkwajuni) | 2,104 | 2,034 | 1,987 |
| Ileje | 2,101 | 2,031 | 1,984 |
| Momba (Chitete) | 2,106 | 2,036 | 1,989 |
| Tunduma | 2,101 | 2,031 | 1,984 |
| **Tabora** | **2,089** | **2,019** | **1,972** |
| Igunga | 2,089 | 2,019 | 1,971 |
| Kaliua | 2,102 | 2,032 | 1,985 |
| Ulyankulu | 2,099 | 2,029 | 1,982 |
| Nzega | 2,099 | 2,029 | 1,982 |
| Sikonge | 2,098 | 2,028 | 1,981 |
| Urambo | 2,099 | 2,029 | 1,982 |
| Uyui | 2,095 | 2,025 | 1,978 |
| **Tanga** | **2,082** | **1,919** | **1,994** |
| Handeni | 2,103 | 1,939 | 2,015 |
| Kilindi | 2,118 | 1,954 | 2,030 |
| Korogwe | 2,094 | 1,931 | 2,006 |
| Lushoto | 2,104 | 1,940 | 2,016 |
| Mkinga (Maramba) | 2,089 | 1,926 | 2,001 |
| Muheza | 2,087 | 1,924 | 1,999 |
| Pangani | 2,089 | 1,925 | 2,001 |

Bei za mafuta katika wilaya zilizopo katika mkoa wa Tabora (isipokuwa Nzega na Igunga) zimekokotolewa kwa kuzingatia umbali wa njia ya sasa iliyojengwa kwa kiwango cha lami (Dar es Salaam – Dodoma- Itigi – Tabora).

## JEDWALI B: BEI ZA JUMLA

| Bandari | Petroli (Shs/Lita) | Dizeli (Shs/Lita) | Mafuta ya Taa (Shs/Lita) |
|---|---|---|---|
| DAR ES SALAAM | 1,852.47 | 1,782.35 | 1,735.69 |
| TANGA | 1,953.45 | 1,790.34 | 1,866.20 |
| MTWARA | 1,775.33 | 1,700.66 | - |

**Gerald M. Maganga**
**Kny: MKURUGENZI MKUU**
**EWURA**